

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**WIZARA YA AFYA**

**TAARIFA KWA UMMA**

## **MLIPUKO WA UGONJWA WA EBOLA NCHINI UGANDA**

**Dodoma, Septemba 21, 2022.**

**Ndugu Wananchi,**

Mnamo tarehe 20 mwezi Septemba, 2022 Wizara ilipata taarifa kuitia vyombo mbalimbali vya habari juu ya mlipuko wa ugonjwa wa Ebola nchini Uganda. Taarifa ilieleza mgonjwa aliyethibitika kuwa na ugonjwa wa Ebola amefariki wilayani Mubende nchini Uganda. Taarifa hizo zilionesha kuwa na dalili za homa kali, degedege, kutapika matapishi yenye damu, kuharisha na kutokwa damu machoni.

Taarifa za uchunguzi zinaonesha ugonjwa huu umesababishwa na kirusi cha Ebola aina ya Sudan (Ebola-Sudan strain). Uwepo wa ugonjwa huu katika nchi jirani unaiweka nchi yetu katika hatari kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu kuitia mipaka ya nchi kavu, viwanja vya ndege na bandari.

**Ndugu Wananchi,**

Dalili kuu za ugonjwa huu ni pamoja na homa kali, inayoambatana na kutokwa damu katika matundu ya mwili yaani pua, njia ya haja kubwa na ndogo, mdomoni, masikioni na machoni, hali inayopelekea kifo kwa muda mfupi. Ugonjwa huu unaenea kwa kugusa majimaji ya mwili wa mgonjwa mfano mate, damu, mkojo na machozi. Endapo utapata au kuona mtu mwenye dalili hizi, unashauriwa kuwahi kituo cha kutolea huduma za afya mapema.

**Ndugu Wananchi,**

Nimewaaagiza Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri nchini kuimarisha utoaji wa elimu, ufuatiliaji wa ugonjwa, uchunguzi wa kitaalam na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba na kinga muhimu katika maeneo yao. Vilevile, nimewaelekeza kuimarisha uchunguzi wa wageni wanaoingia nchini kuititia mipaka yetu ikiwemo matumizi ya vipima joto (thermal scanners).

**Ndugu Wananchi,**

Wizara inapenda kuwajulisha kwamba hadi sasa hakuna mgonjwa wa Ebola nchini. Aidha ninawashauri wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na kunawa mikono kwa maji safi na sabuni, kuepuka kugusa mwili au majimaji ya mwili wa mhiswa au mgonjwa wa Ebola, na kuepuka safari zisizo za lazima kutembelea maeneo yaliyoathirika na ugonjwa huu.



Dkt. Godwin Mollel (Mb)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA**